JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

www.lands.go.tz @wizara_ya_ardhi/ardhiTV

HALIUZWI
JARIDA MAALUM
MARCH 2026



# ARDHI BULLETIN



## Yaliyomo:


13,000 wanufaika na Samia Ardhi Kliniki nchini

Migiro aomba uharakishwaji wa Hati

Kilombero wahimizwa kutumia Samia Ardhi Kliniki


# SAMIA ARDHI KLINIKI



"Jumla ya wananchi 13,550 wamejitokeza kupata huduma mbalimbali za sekta ya ardhi kupitia Samia Ardhi Kliniki iliyofanyika katika mikoa yote 26 nchini".

**Mhe. Dkt. Leonard Akwilapo**
WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

## Migogoro

Katika hatua nyingine, Dkt Akwilapo amesema, kupitia Samia Ardhi Kliniki jumla ya kero, malalamiko na migogoro ya ardhi 707 zimesikilizwa na kupatiwa ufumbuzi, huku Serikali ikikusanya kiasi cha shilingi milioni 972.16 kupitia huduma mbalimbali zilizotolewa katika kliniki hizo.

## Wadau

Waziri Akwilapo pia amewashukuru wadau mbalimbali walioshiriki kufanikisha kliniki hiyo wakiwemo Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Chama cha Wanasheria Wanawake (TAWLA) na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa kushirikiana na Serikali katika kutoa elimu na msaada wa kisheria kwa wananchi.

## Utekelezaji

Samia Ardhi Kliniki ilianza Machi 2, 2026 na kuhitimishwa tarehe 7 Machi 2026 ikiwa ni kuelekea kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambapo Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeanzisha kliniki hiyo kwa lengo kuwafikia wanawake na kuwapatia elimu ya masuala ya ardhi.





## WANANCHI ZAIDI YA 13,000 WANUFAIKA NA SAMIA ARDHI KLINIKI NCHINI

Na Munir Shemweta

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. Dkt. Leonard Akwilapo amesema jumla ya wananchi 13,550 wamejitokeza kupata huduma mbalimbali za sekta ya ardhi kupitia Samia Ardhi Kliniki iliyofanyika katika mikoa yote 26 nchini.

Dkt. Akwilapo amesema hayo wakati akifunga rasmi Samia Ardhi Kliniki katika viwanja vya Mashujaa mkoani Mtwara tarehe 7 Machi 2026, akisema kliniki hiyo imekuwa jukwaa muhimu la kusogeza huduma za ardhi karibu na wananchi hususan wanawake.

Amesema, kati ya wananchi waliojitokeza katika kliniki hizo, wanawake walikuwa 8,725 sawa na asilimia 64.4 huku wanaume wakiwa 3,892 sawa na asilimia 35.7, jambo linaloonesha mwitikio mkubwa wa wanawake katika kutumia fursa zinazotolewa na Serikali.

Aidha, Waziri Akwilapo amesema, jumla ya hatimiliki 3,131 zimetolewa kwa wananchi waliokamilisha taratibu za umilikishwaji wa ardhi ambapo hatimiliki 2,081 sawa na asilimia 57.4 zimetolewa kwa wanawake na hatimiliki 1,543 sawa na asilimia 43.6 zimetolewa kwa wanaume.

Amefafanua kuwa, hatua hiyo imeongeza usalama wa milki kwa wananchi pamoja na kuimarisha uchumi wa familia hususan wanawake kwa kuwaelimisha jambo alilolieza kuwa limelenga kuwawezesha na kulinda haki na kutatua changamoto zao.

“Ardhi ni msingi wa uchumi wa mwananchi na Taifa. Mwanamke anapomiliki ardhi kisheria anapata uwezo mkubwa wa kuwekeza, kufanya shughuli za uzalishaji na hata kupata mikopo katika taasisi za fedha,” alisema.

## TAHARIRI

Samia Ardhi Kliniki iliyoendeshwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuanzia Machi 2 hadi 7, 2026, imefanyika ikiwa ni sehemu ya maandalizi kuelekea kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ikiakisi dhamira ya kuwajengea wanawake uelewa na uwezo wa kumiliki na kusimamia ardhi.

Kupitia kliniki hii, wanawake wamepata fursa ya kupatiwa elimu kuhusu haki za umiliki wa ardhi, taratibu za kupata hati, pamoja na namna ya kutatua migogoro ya ardhi inayowakabili.

Hatua hii ni ya kupongezwa, ikizingatiwa kuwa kwa muda mrefu wanawake wamekuwa miongoni mwa makundi yanayokumbwa na changamoto katika upatikanaji wa haki za ardhi.

Kwa mtazamo wa tahariri hii, Samia Ardhi Kliniki ni mwanzo mzuri wa safari ya kuhakikisha usawa katika umiliki wa rasilimali ardhi, lakini mafanikio yake yatategemea utekelezaji wa hatua za kudumu zitakazowezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya taifa.

**WACHANGIAJI**
Eleuteri Mangi
Munir Shemweta
Lusajo Mwakabuku
Magreth Lyimo
Goodluck Mwihava
Joel Magese
Jeston Kihwelo
Mwanahamisi Mohamed

**Msanifu Kurasa**
Lusajo Mwakabuku

## NAIBU WAZIRI KASPAR MMUYA:
# "WATU WOTE WANA HAKI YA KUMILIKI ARDHI"

Na Joel Magese

Katika Kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake duniani Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Kaspar Mmuya amesema kila mtu anayo-haki ya kumiliki ardhi kwa mujibu wa sheria za nchi.

Naibu Waziri Mmuya amesema hayo mkoani Manyara tarehe 03 Machi 2026 alipotembelea Kliniki ya Ardhi iju-likanayo kama Samia Ardhi Kliniki inayoendelea katika ofi-si za kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Manyara.



"Mwanamke asionekane anamiliki ardhi kwa kuzingatia mila na desturi za kabila lake hapana, sheria ndio iongo-ze katika kumpa haki yake" amesema Naibu waziri Kaspar Mmuya.

Ameongeza kuwa maboresho ya Sera ya Ardhi ya Mwaka 2023 yamelenga kutoa usawa kwa kila mtu kumiliki ardhi mathalani wanawake ambao mifumo ya kiimla imekuwa ikiwaminya wanawake katika haki ya kumiliki ardhi zao.

Kwa upande wake Mpima ardhi wa halmashauri ya Mji wa Babati Bi. Ploskovia Lambert Luta amewataka wananchi kujitokeza kwa wingi katika kliniki hiyo ili waweze kupatiwa hatimiliki zao wakiwa na Nyaraka Stahiki .

Naye Bi. Fatuma Abdallah Bakari Mkazi wa Hangoni C Wilayani Babati Mkoani Manyara ameishukuru Serikali kwa kuwapa kipaumbele wanawake katika kumiliki ardhi ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Ardhi toleo la 2023.

Zoezi la Samia Ardhi Kliniki linaendelea katika mikoa yote nchini kuelekea maadhimisho ya siku ya wanawake duni-ani likilenga kutoa hamasa kwa wanawake nchini kuweza kumiliki ardhi kwa kupatiwa hatimiliki.



> **"Maboresho ya Sera yameondoa vikwazo vya mila na tamaduni vinavyoathiri upatikanaji sawa wa haki ya kumiliki ardhi.**

## KATIBU MKUU WIZARA YA ARDHI
# AZINDUA SAMIA ARDHI KLINIKI DODOMA

Na Magreth Lymo

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mha. Anthony Sanga, amezindua rasmi Samia Ardhi Kliniki mkoa wa Dodoma, ikiwa ni mpango maalumu unaolenga kuongeza asilimia ya umiliki wa ardhi kwa wanawake, ambapo kwa sasa takribani asilimia 28 pekee ya wanawake ndio wanamiliki ardhi.

Hatua hiyo ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, za kuhakikisha huduma za ardhi zinatolewa kwa wananchi kwa kuzingatia misingi ya haki na usawa.

Mha. Sanga aliyasema hayo tarehe 02 Machi, 2026 katika Ofisi ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Dodoma, wakati wa uzinduzi wa Kliniki hiyo maalumu mkoani humo itakayofanyika kwa siku sita kuanzia tarehe 02 hadi 07



Machi, 2026.

Alieleza kuwa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 ilitambua haki sawa katika umiliki wa ardhi, hata hivyo iliacha nafasi ya kuzingatia mila na tamaduni katika taratibu za kumiliki ardhi



hususan kupitia urithi, jambo ambalo kwa baadhi ya makabila limekuwa kikwazo kwa wanawake kupata haki hiyo.

"Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 (toleo la mwaka 2023), iliyozinduliwa rasmi Machi 2025 na Mhe. Rais, imefanyiwa maboresho ikiwemo kuondoa vikwazo vya mila na tamaduni vinavyoathiri upatikanaji sawa wa haki ya kumiliki ardhi, hususan kwa wanawake," alisema Mha. Sanga.

Aidha, alisisitiza kuwa kupitia Samia Ardhi Kliniki, wanawake wanapatiwa huduma mbalimbali ikiwemo elimu na ushauri kuhusu masuala ya ardhi, utoaji wa hati miliki papo kwa hapo, makadirio ya kodi ya pango la ardhi pamoja na huduma nyingine muhimu.



# Kauli Mbiu: Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana; Msingi Jumuishi kufikia Dira 2050.

Aliongeza kuwa mpango huo unalenga kuhakikisha changamoto zinazowakabili wanawake katika sekta ya ardhi zinatatuliwa kwa wakati na kwa ufanisi.

Kwa upande wake, Mthamini Mkuu wa



Serikali wa Wizara hiyo, Bi. Evelyne Baruti Mugasha, alisema hadi majira ya mchana wanawake zaidi ya 160 walikuwa tayari wamejitokeza kupata huduma.

Bi. Mugasha aliwahimiza wanawake wa Mkoa wa Dodoma kutumia fursa ya Kliniki hiyo kupata elimu, ushauri na huduma mbalimbali za ardhi, huku akitoa wito kwa wanaume kutoa ushirikiano ili kuwawezesha wanawake kushiriki kikamilifu.

Wanawake waliopata huduma katika Kliniki hiyo wamepongeza jitihada za Rais Samia kwa kuwapa kipaumbele wanawake katika upatikanaji wa hati



miliki ili kuhakikisha hawabaki nyuma kimaendeleo.

Mkazi wa Ilazo, Zena Hamis, alimshukuru Rais Samia kwa kuwapa wanawake kipaumbele na kuwasihi wanawake wote wenye uhitaji wa huduma za ardhi kujitokeza kwa wingi kabla ya Kliniki hiyo kufikia tamati.

# WIZARA YA ARDHI YAWALENGA WANAWAKE KUPITIA MPANGO WA ''SAMIA ARDHI KLINIKI''

Na Lusajo Mwakabuku

Wanawake maelfu nchini wamenufaika na huduma za elimu, ushauri na urasimishaji wa haki za ardhi kupitia mpango maalum wa "Samia Ardhi Kliniki" uliotekelezwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara kuanzia tarehe 2 hadi 7 Machi 2026, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Mpango huo ulihusisha utoaji wa huduma mbalimbali ikiwemo uhakiki wa nyaraka za ardhi, usajili wa hati, utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa njia ya usuluhishi, pamoja na utoaji wa elimu ya sheria za ardhi hususan kwa wanawake. Aidha, wataalamu wa sekta ya ardhi walifika moja kwa moja katika maeneo ya wananchi ili kurahisisha upatikanaji wa huduma hizo bila wananchi kulazimika kufika ofisini.

Akizungumza na waandishi wa habari, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Lucy Kabyemera, alisema kliniki hiyo ililenga kuongeza uelewa wa wanawake kuhusu haki yao ya kumiliki ardhi na kuwawezesha kupata nyaraka halali za umiliki kwa urahisi zaidi.

Alieleza kuwa maadhimisho ya Siku ya Wanawake

**"Siku ya Wanawake Duniani hufanyika kila mwaka tarehe 8 Machi kwa mujibu wa Maazimio ya Beijing ya mwaka 1995, na mwaka 2026 yaliadhimishwa kwa kaulimbiu isemayo: "Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana; Msingi Jumuishi kufikia Dira 2050."**



Duniani hufanyika kila mwaka tarehe 8 Machi kwa mujibu wa Maazimio ya Beijing ya mwaka 1995, na mwaka 2026 yaliadhimishwa kwa kaulimbiu isemayo: "Haki na Usawa kwa Wanawake na Wasichana; Msingi Jumuishi kufikia Dira 2050."

Kwa mujibu wake, utekelezaji wa kliniki hiyo ulitokana na maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ambaye amekuwa akisisitiza umuhimu wa kusogeza huduma karibu na wananchi na kuhakikisha makundi yote, hususan wanawake, yanapata fursa sawa katika rasilimali za ardhi.

Bi. Kabyemera alibainisha kuwa kupitia kaulimbiu



mahsusi ya kliniki hiyo, "Mwanamke; Haki Yako, Miliki Ardhi Sasa," wanawake wengi walihamasika kujitokeza na kunufaika na huduma hizo, hali iliyochangia kuongeza mwamko wa ushiriki wao katika masuala ya umiliki wa ardhi.

Aidha, alieleza kuwa maboresho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 (toleo la 2023) yameendelea kuondoa vikwazo vya kimfumo na kijamii, ikiwemo mila na desturi zilizokuwa zinawakwamisha wanawake kumiliki ardhi.

Takwimu zinaonesha kuwa kabla ya jitihada hizo, ni takriban asilimia 28 pekee ya wanawake nchini walikuwa wanamiliki ardhi, hali inayoonesha umuhimu wa kuendelea kuimarisha mikakati ya utoaji elimu na huduma rafiki kwa wanawake.










Bi. Kabyemera aliwataka wanawake kuendelea kutumia fursa zinazotolewa na Serikali kupata haki zao za ardhi, huku akitoa wito kwa jamii, hasa wanaume, kuunga mkono juhudi hizo kwa kuwawezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika umiliki na matumizi ya ardhi.

Alisisitiza kuwa kumwezesha mwanamke kumiliki ardhi si tu kunaleta usawa wa kijinsia, bali pia ni kichocheo muhimu cha maendeleo ya uchumi wa familia na taifa kwa ujumla.



# BALOZI DKT MIGIRO AOMBA UHARAKISHWAJI UTOAJI WA HATI ZA ARDHI

Na Lusajo Mwakabuku

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dkt. Asha-Rose Migiro, ameiomba Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhakikisha mchakato wa utoaji wa hati za ardhi unafanyika kwa haraka ili kuwasaidia wananchi kumaliza changamoto za umiliki wa ardhi kwa wakati.

Akizungumza wakati wa utoaji wa huduma za ardhi kwa wananchi katika Samia Ardhi Kliniki Jijini Dar es salaam, Balozi Dkt. Migiro alisema kuwa tayari maelekezo ya kuharakisha upatikanaji wa hati yalitolewa na Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye alitaka taratibu za kupata hati zisichukue muda mrefu.

Alisema wananchi wengi waliokamilisha taratibu zote au wanaoendelea na mchakato wanapaswa kusaidiwa kukamilisha hatua zinazofuata kwa haraka, bila kucheleweshwa pasipo sababu za msingi.

“Mheshimiwa Rais alielekeza kuwa utaratibu wa kupata hati usichukue muda mrefu. Tunafahamu wizara inafanya kazi hiyo, lakini tunaomba barua za ofa zisichukue muda mrefu kutolewa kama hakuna changamoto nyingine,” alisema Migiro.



Aidha, alikumbusha kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Dkt. Leonard Akwilapo tayari alitoa maelekezo hayo alipokuwa Dodoma, akisisitiza kuwa wananchi wanapaswa kupata hati zao ndani ya muda mfupi, na kwamba utekelezaji umeanza katika baadhi ya maeneo.

Katika hatua nyingine, Migiro aliwataka wananchi kuwa na subira wakati wa kushughulikia migogoro ya ardhi, akieleza kuwa changamoto hizo mara nyingi huchukua muda kuzitatua kutokana na taratibu za kisheria na kiutawala.

Alisema hata yeye binafsi anakabiliwa na changamoto ya mgogoro wa ardhi, jambo linalomfanya kuelewa vizuri hali wanayopitia wananchi wengi.

“Hata mimi mama yenu hapa nina mgogoro wa ardhi na nimekuja kupata huduma. Migogoro ipo, kama vile vikombe vinapokaa pamoja haviwezi kuacha kugongana. Muhimu ni kusikilizana na kutatua migogoro hiyo kwa amani,” alisema.

Pia alimpongeza Rais Samia kwa kuanzisha utaratibu wa kuwafuata wananchi na kusikiliza changamoto zao moja kwa moja kupitia utoaji wa huduma za ardhi, akisema hatua hiyo inaonesha dhamira ya serikali ya kuwajali wananchi.

Alisema utaratibu huo unaonesha wazi kuwa serikali ni sikivu na inaendelea kutafuta njia za kutatua changamoto zinazowakabili wananchi katika sekta ya ardhi.

# SAMIA ARDHI KLINIKI YAHAMASISHA WANAWAKE KUMILIKI ARDHI SIMIYU

Na Eleuteri Mangi

Serikali kupitia Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeanzisha Kliniki Maalumu ya Wanawake "Samia Ardhi Kliniki" hatua inayoweka mazingira rafiki kwa wanawake wengi kumiliki ardhi kisheria sambamba na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na maendeleo.

Wanawake wa Mkoa wa Simiyu ambao ni miongoni mwa wanufaika wa kliniki hiyo wameishukuru Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kuwapelekea Samia Ardhi Kliniki inayoendelea kuwahudumia wanawake na kutatua changamoto zinazowakabili katika umiliki wa ardhi katika maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Kliniki hiyo Machi 4, 2026 mjini Bariadi, Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mhe. Anamringi Macha amesema, Kliniki hiyo imekuja muda muafaka kwa kuwa itasaidia wanawake wa mkoa huo kumiliki ardhi na kupata Hati Miliki zao.

Akitoa taarifa ya utendaji kazi wakati wa ufunguzi wa Kliniki hiyo, Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Simiyu Bw. Denis Masami amesema, hadi kufikia Machi 4, 2026 wametoa jumla ya Hati 198 na kuweka bayana kuwa, kliniki hiyo inayotarajiwa kuhitimishwa Machi 7, 2026 ni sehemu ya kuelekea maadhimisho Siku ya Kimataifa ya Wanawake ambayo huadhimishwa kila mwaka Machi 08.




**"Simiyu tuna lengo la kutoa hati 3,000 kwa mwaka 2025/2026 ambapo hadi sasa tumetoa jumla ya hati 1,441 sawa na asilimia 48 ya lengo ambapo kati ya hati hizo 403 ni za wanawake sawa na asilimia 28 ya hati zote zilizotolewa katika mkoa wetu"**

Ameongeza kuwa, Mkoa wa Simiyu una lengo la kutoa hati 3,000 kwa mwaka 2025/2026 ambapo hadi sasa wametoa jumla ya hati 1,441 sawa na asilimia 48 ya lengo ambapo kati ya hati hizo 403 ni za wanawake sawa na asilimia 28 ya hati zote zilizotolewa katika mkoa huo.

Kwa upande wake Bi. Stela Manyonyi kutoka Wilaya ya Busega mkoani Simiyu ameahidi kuitumia hati aliyoipata katika shughuli za maendeleo kwa kuchukulia mkopo wa kuendeleza biashara zake.

Kaulimbiu ya maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake mwaka huu ya inahimiza "Haki sawa kwa Wanawake na Wasichana; Msingi Jumuishi kifikia Dira 2050" huku Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi ikisisitiza kuwa "Mwanamke; Haki Yako, Miliki Ardhi Sasa".




# KILOMBERO WAHIMIZWA KUTUMIA SAMIA ARDHI KLINIKI KUTATUA CHANGAMOTO ZA ARDHI

Na Goodluck Mwihava

Mkuu wa wilaya ya Kilombero mkoani Morogoro Mhe. Wakili Dustan Kyobya amewahimiza wanawake katika Mji wa Ifakara mkoani Morogoro kuhakikisha wanatumia Samia Ardhi Kliniki katika kutatua changamoto za ardhi.

Mhe. Wakili Kyobya ametoa kauli hiyo wakati akizindua Samia Ardhi Kliniki katika Ofisi ya Kata ya Viwanja Sitini Halmashauri ya Mji Ifakara mkoani Morogoro tarehe 3 Machi 2026 ikiwa ni katika Maadhimisho ya Wiki ya Wanawake Duniani ambayo kila mwaka huadhimishwa tarehe 8 Machi.

Lengo la Kliniki hiyo ni kushughulikia masuala mbalimbali ikiwemo Kusikiliza, Kutatua Kero na Migogoro ya Ardhi, kuandaa na Kugawa hatimiliki, kutoa Elimu na Ushauri wa Masuala ya ardhi katika Wiki ya Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Kauli Mbiu kuelekea siku ya Wanawake Duniani katika Samia Ardhi Kliniki ni “Mwanamke Miliki Ardhi yako Sasa, Haki yako” ambapo Mkuu wa Wilaya Mhe. Dunstan Kyobya aliwataka Wananchi kutumia fursa hiyo kwa wenye Kero na changamoto zote za Ardhi wahakikishe zinatatuliwa.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji Ifakara Mhe. Kassim Faya Nakapala alieleza kuwa, Samia Ardhi Kliniki imekuwa tiba na majibu ya changamoto zote za Ardhi katika Mji wa Ifakara na kuwataka Wananchi kuondokana na kasumba ya kutomaliza Migogoro au Kuibua Migogoro ambayo ilikwishapatiwa majibu hata miaka 10 iliyopita.

Naye, Kamishna wa Ardhi Msaidizi Utawala wa Ardhi Bi. Hellen Philip aliahidi kuhakikisha Samia Kliniki Ardhi inawafikia kwa ukaribu na kutoa Huduma kwa weledi Ili kila mwananchi apate tabasamu.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Ifakara Bi. Pilly Kitwana alimshukuru Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwapa tabasamu Wananchi wa Ifakara kwa kuhakikisha Wanawake wanamiliki Ardhi zao lengo ikiwa ni kuongeza umiliki wa Ardhi kwa Wanawake katika nchi yetu.

“Niwahamasishe Wanawake wenzangu pamoja na kina baba na Wananchi wote wa Ifakara tutumie fursa hii muhimu,Migogoro na changamoto za Ardhi zitapatiwa ufumbuzi”.

Alisema Bi.Kitwana

Mmoja wa Mwananchi aliyepata Hati katika Kliniki hiyo Bi. Neema Msango alishukuru Samia Kliniki Ardhi kwa kumpatia Hati na kuwahimiza Wanawake na wananchi kujitokeza kwa wingi kupata huduma za ardhi



# MUFTI MKUU
## AHAMASISHA MATUMIZI YA FURSA ZA ARDHI KWA WANAWAKE

Na Lusajo Mwakabuku

Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Abubakar Zubeir, ametoa wito kwa Watanzania kujitokeza kwa wingi kutumia fursa ya huduma za ardhi zinazotolewa kupitia Samia Ardhi Kliniki, akisisitiza umuhimu wa wanawake kumiliki ardhi kama njia ya kujikomboa kiuchumi.

Mufti Zubeir alitoa kauli hiyo baada ya kufika katika Kliniki ya Ardhi inayofanyika katika Ofisi za Ardhi za Mkoa wa Dar es Salaam, ambapo alipata hati ya ardhi huku akishuhudia namna wananchi wanavyohudumiwa katika kliniki hiyo ambayo inaendelea nchi nzima.

Akizungumza mara baada ya kupata huduma hiyo, Mufti Zubeir alisema hatua ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuandaa Samia Ardhi Kliniki yenye kulenga kuwapa kipaumbele wanawake ni jambo muhimu linalosaidia kuongeza usawa katika umiliki wa rasilimali muhimu kama ardhi.

Alisema wanawake wanapaswa kutumia kikamilifu fursa hiyo ili waweze kupata hati za ardhi na kujiimarisha kiuchumi.

"Wanawake wana haki ya kumiliki mali mbalimbali ikiwemo magari na mali nyingine, hivyo hakuna sababu ya kuwanyima nafasi ya kumiliki ardhi. Ni muhimu jamii, hususan wanaume, kuachana na mila kandamizi zinazowazuia wanawake kumiliki rasilimali," alisema Mufti Zubeir.

Aidha, aliwataka wanaume kuwapa nafasi wanawake kumiliki ardhi ili kuongeza idadi ya wanawake wenye umiliki rasmi wa ardhi nchini, jambo ambalo litasaidia kuimarisha ustawi wa familia na jamii kwa ujumla.

Katika hatua nyingine, Mufti Zubeir alipongeza maandalizi mazuri yaliyofanywa na Ofisi ya Mkoa wa Dar es Salaam katika uendeshaji wa kliniki hiyo, kuanzia mapokezi hadi utoaji wa huduma kwa wananchi.

Alisema namna wateja wanavyohudumiwa kwa ufanisi ni jambo jema lenye manufaa kwa jamii na lina thawabu kubwa mbele za Mwenyezi Mungu, hususan katika kipindi hiki cha mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Mufti Zubeir pia aliwaombea heri watumishi wanaotoa huduma katika kliniki hiyo ili waendelee kuwahudumia wananchi kwa uadilifu na bidii.



# SERIKALI YAHIMIZA UWAJIBAKAJI SEKTA YA ARDHI



Na Munir Shemweta

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. Dkt. Leonard Akwilapo, alitumia uzinduzi wa "Samia Ardhi Kliniki" jijini Dar es Salaam kutangaza msimamo mkali wa Wizara dhidi ya vitendo vya uzembe na ucheleweshaji wa huduma kwa wananchi.

Katika hafla hiyo, Waziri Akwilapo amesema Wizara imeamua "kujivua gamba" na kuanza ukurasa mpya wa uwajibikaji, akisisitiza kuwa kauli za watumishi kudai mafaili kupotea au kutoonekana hazitavumiliwa tena.

"Hakuna kitu kama faili kupotea. Ofisi zetu zina mifumo thabiti, na mafaili hayana miguu ya kutoroka. Kauli hizi

Waziri huyo alieleza kuwa hatua hiyo ni sehemu ya mageuzi yanayolenga kurejesha imani ya wananchi kwa sekta ya ardhi, ambayo imekuwa ikikabiliwa na malalamiko ya muda mrefu kuhusu urasimu na usumbufu usio wa lazima.

Alisema Wizara haitasita kuchukua hatua kali za kinidhamu kwa watumishi watakaobainika kukwamisha huduma kwa maslahi binafsi, akisisitiza kuwa ardhi ni rasilimali ya Taifa na watumishi ni wasimamizi tu, si wamiliki.

Uzinduzi wa "Samia Ardhi Kliniki" umefanyika ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan. Kliniki hiyo itafanyika nchi nzima kuanzia Machi 2 hadi 7, 2026, ikitoa huduma za msaada wa kisheria, utoaji wa hatimiliki na elimu ya taratibu za umilikishwaji wa ardhi.

Mbali na kuhimiza wanawake kujitokeza kunufaika na huduma hizo, Waziri Akwilapo aliwataka wanaume na viongozi wa kaya kuachana na mila potofu zinazowanyima wanawake haki ya kumiliki ardhi.

Kwa mujibu wa Waziri, idadi ya wanawake wenye hatimiliki imeongezeka hadi wastani wa asilimia 28 kutoka chini ya asilimia 10 miaka ya nyuma, hatua

aliyoitaja kuwa ni mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita.

Kauli mbiu ya zoezi hilo ni: "Mwanamke; Haki Yako, Miliki Ardhi Sasa," ikiwa ni sehemu ya mkakati mpana wa kuhakikisha usawa wa kijinsia na kuimarisha uchumi wa familia na Taifa kwa ujumla.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Ilala Bw Edward Mpogolo akimuwakilisha Mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam Bw. Albert Chalamila mbali na kuipongeza Wizara ya Ardhi kwa kuanzisha Samia Ardhi Kliniki, amesema kuna baadhi ya changamoto zilizoanza kujitokeza kwa wale wanaopata hati miliki za ardhi kufunga barabara zinazotumika kwa jamii.

Aliomba utaratibu wa fomu za kuthibitishwa na majirani katika maeneo yaliyorasimishwa kuzingatiwa kwa kupitishwa katika ngazi husika na kusimamiwa ili kuepuka changamoto

**"Hakuna kitu kama faili kupotea. Ofisi zetu zina mifumo thabiti, na mafaili hayana miguu ya kutoroka»**

kama hizo

# HAKI YAPATIKANA KWA MJANE KUPITIA SAMIA ARDHI KLINIKI

Na Mwanahamis Mohamed

Kampeni ya Samia Ardhi Kliniki inaendelea kuleta matumaini kwa wananchi wengi hususan wanawake waliokuwa wakikabiliwa na changamoto mbalimbali za ardhi nchini.

Katika Kijiji cha Ifucha, Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, tarehe 5 Machi 2026, familia ya mama mjane Bi. Habiba Mzee imeelezea furaha yake baada ya kufanikiwa kupata haki kwenye ardhi iliyokuwa ikitishiwa kunyang'anywa na watu wenye nia ovu.

Changamoto hiyo imepata suluhisho kupitia Samia Ardhi Kliniki, hatua iliyorejesha matumaini sambamba na kuimarisha umiliki wa ardhi waliyoimiliki kwa muda mrefu na hivyo kuiwezesha familia hiyo kuendelea na shughuli zao za maendeleo kwa utulivu bila hofu ya kupoteza mali yao.

Akizungumza baada ya kupatiwa ufumbuzi wa changamoto hiyo, mjane huyo mkazi wa Kitete, Tabora, Bi. Habiba Mzee, alimshukuru Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Tabora, Bw. Tumaini Gwakisa, kwa weledi na uvumilivu wake katika kusikiliza na kutatua changamoto za wananchi kwa haki.

Aidha, ametoa wito kwa wananchi wengine wenye changamoto za ardhi kujitokeza katika Samia Ardhi Kliniki ili kupata msaada wa kitaalamu kutoka kwa wataalamu wa sekta ya ardhi wanaotoa huduma hiyo.



**"Namshukuru Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Tabora, Bw. Tumaini Gwakisa, kwa weledi na uvumilivu wake katika kusikiliza na kutatua changamoto za wananchi kwa haki. kwa wananchi wenzangu wenye changamoto jitokezeni katika Samia Ardhi Kliniki ili mpate msaada"**

Bi. Habiba Mzee - Mjane

# SAMIA ARDHI KLINIKI YAGUSA MAISHA YA WANAWAKE SINGIDA

Na Jeston Kihwelo

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhandisi Antony Sanga, amegawa zaidi ya hati miliki 50 za ardhi kwa wanawake mkoani Singida kupitia zoezi la Samia Ardhi Kliniki, huku akiwahamasisha wanawake kujitokeza kumiliki ardhi ili kujiletea maendeleo binafsi na ya familia zao.

Akizungumza Machi 5, 2026 katika Ofisi ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Singida, Mhandisi Sanga alisema, Wizara ya Ardhi chini ya Waziri Dkt. Leonard Akwilapo imejipanga kuongeza idadi ya wanawake wanaomiliki ardhi nchini kwa kuendelea kutoa elimu na huduma za ardhi kwa wananchi.



Alisema Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 (Toleo la 2023) inatoa haki sawa kwa wanawake na wanaume kumiliki ardhi, hivyo wizara inaendelea kuhamasisha utekelezaji wake na kuwataka watumishi wa sekta ya ardhi nchini kuhakikisha wanawake wanapata huduma bila ubaguzi.

Kwa upande wake, Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Singida Bi. Shamim Hoza alisema kupitia Samia Ardhi Kliniki, wanawake 144 na wanaume 36 wamepatiwa huduma mbalimbali za ardhi, migogoro 18 imepokelewa na 10 kutatuliwa, viwanja



18 vimepimwa, zaidi ya milioni 23 zimekusanywa kama ada na hati Zaidi ya 50 zimetolewa wanawake huku zaidi ya wanawake 1,350 wakipatiwa elimu ya masuala ya ardhi.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Singida Godwin Gongwe, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa Halima Dendego, alieleza kuwa, ujio wa Samia Ardhi Klinkwani zaidi ya kesi 900 za ardhi zimeanza kushughulikiwa kupitia Kikosi Kazi cha SAMIA, huku akibainisha kuwa wanawake ndio waathirika wakubwa wa migogoro ya ardhi hivyo wanahitaji kuendelea kupewa elimu na haki zao.

Akizungumza kwaniaba ya wanawake walioshiliki samia Ardhi kliniki Mkoani Singida Bi Aisha Mohamed eliishukuru wizara ya Ardhi kwa kuwaletea Samia Ardhi Kliniki mkoa wa Singida kwaani imewanufaisha wanawake wengi kupitia upimaji wa maeneo yao,kupatiwa Hati miliki na kuwaongezea uelewa kuhusu masuala ya Miliki za Ardhi.

Kamishna Mkuu Msaidizi wa Ardhi Bw. Hussein Sadiki, Katibu Tawala Msaidizi upande wa Miundombinu Bw. Kirina Domicianus aliyemwakilisha Katibu Tawala wa Mkoa ni miongoni Viongozi walioshiriki Hafla ya Ugawaji wa Hati na utoaji wa elimu ya Masuala ya Ardhi katika Samia Ardhi Kliniki Mkoani Singida.





"MWANAMKE; HAKI YAKO, MILIKI ARDHI SASA"

# SENYAMULE AIPA KONGOLE WIZARA YA ARDHI

Na Magreth Lyimo

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule amepongeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kuendesha zoezi la Samia Ardhi Kliniki linalofanyika nchi nzima.

Mhe. Senyamule ametoa pongezi hizo leo Machi 5, 2026 alipotembelea kliniki hiyo inayoendelea katika viwanja vya Ofisi ya Kamishna wa Ardhi  Msaidizi Mkoa wa Dodoma.

“Nimekaa sijawahi kuona ubunifu wa jambo hili, na nimeambiwa linafanyika nchi nzima ya Tanzania. Hiki ni kitu cha pekee sana,” amesema Senyamule.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa mkoa wa Dodoma, awali aliposikia kuhusu kliniki hiyo alijiuliza kama kutapatikana wanawake wa kutosha kwenda kutatuliwa  kero zao za ardhi, lakini hali imekuwa tofauti.

“Nilijiuliza kama wanawake watapatikana kwa wingi, lakini leo nimeshangaa kuona na kushuhudia kuwa sasa wanawake wengi wanamiliki ardhi,” amesema Senyamule.

Aidha, amesema kuwa kama jambo hilo lingefanyika miaka kumi au ishirini iliyopita, isingekuwa rahisi kupata wanawake wengi kwa sababu wengi hawakuwa na uelewa wa haki yao ya kumiliki ardhi.

“Kama ungelifanya jambo hili miaka kumi au ishirini iliyopita na kusema wanawake waje washughulikie kero zao za ardhi na kupata hati, usingewapata wengi kwa sababu wakati huo hatukuwa na uelewa kuwa sisi pia tunastahili kumiliki ardhi,” ameongeza.



SAMIA ARDHI KLINIKI

Katika hatua nyingine, Mhe. Senyamule amewaasa wanawake kutunza vizuri hati zao za ardhi, akieleza kuwa ardhi ya Dodoma ina thamani kubwa inayoongezeka kila siku.

“Ukishapata hati yako, itunze vizuri kwa sababu ardhi ya Dodoma ina thamani kubwa na thamani yake inaendelea kuongezeka kila siku,” amesema.

Sambamba na hilo, Mhe. Senyamule pia alikabidhi hati miliki kwa baadhi ya wanawake waliofika katika kliniki hiyo iliyofanyika katika viwanja vya Ofisi ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Dodoma.

Samia Ardhi Kliniki ilianza rasmi tarehe 2 Machi 2026 katika mikoa yote nchini na kuhitimishwa tarehe 7 Machi 2026 yenye Kauli Mbiu, Mwanamke; Haki Yako, Miliki Ardhi sasa.

# JUWAKITA WAISHUKURU WIZARA YA ARDHI KUTATUA MGOGORO ULIODUMU KWA MUDA MREFU

Na Jeston Kiwhelo




Jumiya ya Wanawake wa Kiislamu (JUWAKITA) Wilaya ya Singida na mkoa wameishukuru Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kufanikisha utatuzi wa mgogoro wa ardhi uliodumu kwa muda mrefu katika eneo lao la Manga lililopo Kata ya Mtipa, Manispaa ya Singida.

Akizungumza baada ya kupatikana kwa suluhu ya mgogoro huo, Mwenyekiti wa JUWAKITA Wilaya alisema, wanaipongeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Singida kwa juhudi zilizowezesha kutatua mgogoro uliokuwa baina ya taasisi yao, wawekezaji pamoja na baadhi ya wananchi wa eneo hilo.

Amesema, mgogoro huo uliidumu kwa muda mrefu uliweza kupatiwa ufumbuzi baada ya viongozi wa wizara kufika na kusikiliza pande zote zinazohusika, hatua iliyosaidia kurejesha amani na uelewano katika eneo hilo.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhandisi Anthony Sanga amewapongeza wanawake hao kwa kujitokeza kwa wingi kushiriki zoezi la Samia Ardhi Kliniki linaloendelea mkoani Singida.

Amesema, serikali inaendelea kusikiliza na kutatua migogoro ya ardhi ili kuhakikisha haki inapatikana kwa wananchi wote, huku akiwapa pole wanawake hao kwa usumbufu walioupata kutokana na mgogoro huo wa muda mrefu.


# BIBI MIAKA 95 ATOA SOMO LA UMILIKI HALALI WA ARDHI

Na Jeston Kihwelo

Eliselina Watson Mwashinga, bibi mwenye umri wa miaka 95 amekuwa gumzo mkoani Mbeya baada ya kujitokeza katika Samia Ardhi Kliniki na kufanikisha kukamilisha taratibu za umilikishaji wa hati ya ardhi yake, hatua iliyowagusa na kuwavutia wananchi wengi waliokuwepo.

Akiwa na dhamira thabiti ya kuhakikisha anamiliki ardhi yake kihalali, bibi huyo alifika kliniki hapo na kulipia gharama stahiki pamoja na kuchukua hati yake. Kutokana na umri wake mkubwa, hakuweza kusaini kwa mkono, hivyo alisaidiwa na wataalamu kwa kutumia alama ya dole (fingerprint) kukamilisha mchakato huo kwa usalama na ufanisi.

Tukio hilo limekuja wakati Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ikiendelea na utekelezaji wa Samia Ardhi Kliniki iliyoanza rasmi tarehe 02 hadi 07 Machi 2026. Kliniki hiyo imelenga kutoa huduma za umiliki wa ardhi hususan kwa wanawake, ikiwa ni sehemu ya maandalizi na maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yanayoadhimishwa kila mwaka tarehe 8 Machi.



Kupitia mpango huo maalum, wanawake wanapatiwa fursa ya kusajili, kuhamisha na kukamilisha taratibu za hati za ardhi kwa urahisi zaidi, sambamba na kupata elimu juu ya haki zao za kumiliki mali. Hatua hiyo inalenga kuimarisha usawa wa kijinsia katika umiliki wa ardhi na kuwawezesha wanawake kiuchumi kupitia umiliki salama na halali wa rasilimali hiyo muhimu.

Wananchi walioshuhudia tukio hilo walieleza kuvutiwa na uthubutu wa bibi huyo, wakisema ametoa funzo kwa jamii kuwa hakuna umri wa kuchelewa kuweka mambo yako ya ardhi katika utaratibu wa kisheria. “Ametuhamasisha sana. Kama yeye katika umri huo ameweza, sisi hatuna sababu ya kusubiri,” alisema mmoja wa wananchi.

Kwa upande wake Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Mbeya Bi Syabumi Mwaipopo amempongeza Bibi huyo kwa hatua na uthubutu huo, akisisitiza kuwa huduma katika kliniki hiyo zinalenga kuwafikia wananchi wote, wakiwemo wazee na makundi maalum, kwa urahisi na heshima.

Hatua ya bibi huyo wa miaka 95 imeelezwa kuwa kielelezo cha mafanikio ya mkakati wa Wizara wa kusogeza huduma karibu na wananchi na kuhamasisha wanawake kujitokeza kumiliki ardhi kihalali. Tukio hilo limebeba ujumbe mzito kwamba umiliki wa ardhi si suala la umri, bali ni haki na wajibu wa kila mwananchi anayejali mustakabali wa mali na familia yake.

# HABARI PICHA

## ZA SAMIA ARDHI KLINIKI NCHINI























# JINSI YA KUJISAJILI KWENYE MFUMO

e-Ardhi
Huduma Chap!


Mwanzo | Verify Documents | Ingia | Jisajili

# e-ARDHI


### 1. NAMNA YA KUJISAJILI KWENYE MFUMO WA eARDHI

**Fuata hatua hizi muhimu:**

1. Fungua tovuti: https://eardhi.lands.go.tz
2. Bonyeza "Jisajili" (Create Account)




3. Jaza taarifa binafsi:
   - Namba ya NIDA
   - Namba ya simu



4. **Pokea OTP** (One Time Password) kwenye namba ya simu uliyoingiza.
5. Ingiza namba hizo (OTP) ili kuendelea.
6. Weka taarifa zako zaidi (mfano, barua pepe na nywila mpya).
   - **Mfano wa nywila salama:** *Mkombozi@2025* (mchanganyiko wa herufi na alama).
7. Bonyeza "**Jisajili**" ili kukamilisha usajili.

### 2. NAMNA YA KUINGIA KWENYE MFUMO (LOGIN)

1. Tembelea https://eardhi.lands.go.tz




2. Bonyeza "**Ingia**".
3. Chagua njia ya kuingia (Namba ya simu, NIN, NIDA au barua pepe).
4. Weka:
   - Jina la mtumiaji (barua pepe au namba ya simu au NIDA).
   - Nywila (Password).
5. Bonyeza "**Ingia**" ili kufungua akaunti yako.

### JINSI YA KUOMBA HUDUMA NDANI YA MFUMO


1. Ingia kwenye akaunti yako.
2. Chagua "Maombi"
3. Chagua huduma unayotaka (mfano: "OmbaHatimiliki").
4. Bonyeza alama ya + (jumlisha) kisha jaza fomu ya maombi.
5. Ambatanisha nyaraka.
6. Thibitisha taarifa na bonyeza "Tuma".
7. Subiri ujumbe wa uthibitisho au maelekezo zaidi.

### 3. JINSI YA KUBADILI NYWILA (PASSWORD RESET)

1. Tembelea https://eardhi.lands.go.tz.
2. Bonyeza "**Ingia**".
3. Chagua "**Badili Nywila**".



4. Ingiza taarifa (NIN, barua pepe au namba ya simu) kulingana na chaguo lako.



5. Bonyeza "**Badili Nywila**".
6. Fungua simu/barua pepe yako upate ujumbe wenye link ya kuweka nywila mpya.
7. Tumia nywila mpya kuingia tena kwenye mfumo wa e-Ardhi.

**Unaweza pia kufuatilia hali ya ombi lako kwa kubonyeza vidoti vitatu vilivyo upande wa kulia wa muamala husika.**

### JINSI YA KUFUATILIA MAOMBI YAKO

1. Ingia kwenye akaunti yako. Bonyeza "Maombi".
3. Utaona taarifa za:
   - Hali ya maombi
   - Hatua inayofuata.
   - Malipo au nyaraka zinazokosekana.

Taarifa pia zinaweza kukufikia kupitia SMS au barua pepe.

### WASILIANA NASI:

**Simu: 0717722449 /071468162/ 0625652O84/0755762375/0713986261**
**Email: support@lands.go.tz**
**Tovuti: https:/eardhi. lands.go.tz**
**Au tembelea ofisi ya ardhi ya wilaya au mkoa wako kwa msaada zaidi.**

Karibu tukuhudumie!